

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA




# BAJETI YA SERIKALI YA MWAKA 2011/2012 TOLEO LA WANANCHI

Imetolewa na Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Policy Forum

policy forum




# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA FEDHA

## BAJETI YA SERIKALI YA MWAKA 2011/2012
## TOLEO LA WANANCHI

**Imetolewa na Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Policy Forum**

## 1. Bajeti ya Mwananchi

Bajeti ya Mwananchi ni bajeti iliyorahisishwa na ambayo imewekwa katika muundo unaomfanya mwananchi wa kawaida aweze kuelewa mambo muhimu ambayo Serikali imeyapanga katika mwaka wa fedha. Bajeti hii ya mwananchi inalenga kufanya taarifa za kifedha zieleweke kwa urahisi na mwananchi wa kawaida na kuwapa wananchi fursa ya kuelewa mipango ya Serikali na mchakato wa kutekeleza bajeti hiyo. Bajeti inataja kwa ufupi wapi Serikali itapata fedha na jinsi ilivyojipanga kutumia fedha hizo.

Mwaka wa fedha wa 2011/2012 ni mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano wa Serikali ambao unahusisha nguzo tano:

- Kuendeleza uwezo wa utengemavu wa uchumi jumla na kudumisha mafanikio yatayopatikana katika kutoa huduma za jamii,
- Kutumia rasilimali zilizopo kama kichocheo cha kukuza uchumi,
- Kutumia fursa ya kijiografia ya Tanzania, na
- Kuongezeka kwa matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Kwa msingi huo, Bajeti ya mwaka 2011/2012 imelenga kutatua pamoja na mambo mengine, changamoto zifuatazo:

- Kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani kupitia ongezeko la uwekezaji wa Serikali katika vichocheo vya uchumi hali kadhalika na kupanua msingi wa kodi.
- Kupanda kwa gharama za maisha na kiwango kikubwa cha ukosefu wa ajira kati ya vijana ambao unasababishwa na ongezeko la bei za bidhaa na huduma mbalimbali na kiwango kidogo cha ajira.

## 2. Serikali inataka kufanikisha nini katika mwaka 2011/2012

Kwa ujumla, Bajeti hii imelenga kuchukua hatua za kupunguza gharama za maisha kwa wananchi na kuchochea ukuaji wa uchumi kwa kutekeleza yafuatayo:-

A. Kuongeza ubora wa huduma za Afya na Elimu nchini kupitia:

- Kudumisha faida na mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya afya na elimu, kuboresha upatikanaji wa huduma bora zinazotolewa na sekta hizi.

B. Kuboresha tija katika uzalishaji wa mazao ya Kilimo na mfumo wa Umwagiliaji kupitia:

- Kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi katika Kilimo,
- Kuimarisha Utafiti na kukuza/kuendeleza uzalishaji katika kilimo na teknolojia za matumizi ya mashine katika kilimo,
- Kuboresha miundombinu iliyopo ya hifadhi ya taifa ya chakula na kuanzisha vituo vingine katika maeneo muhimu,
- Kujenga vituo muhimu vya kuhifadhia maji (yaani; mabwawa madogo, ya kati na makubwa), umwagiliaji na miundombinu ya kupitisha maji kwa ajili ya skimu 33,
- Kukarabati skimu za umwagiliaji za asili zilizopo, na vyama vya msingi vya ushirika,
- Kuendeleza na kuimarisha mashirika ya Umma.

C. Kuboresha miundombinu ya barabara na usafirishaji (barabara,reli, bandari, viwanda vya ndege na mkongo wa taifa wa mawasiliano) kupitia:

- Kukarabati reli kama vile za TAZARA na reli ya kati,
- Kukarabati na kupanua viwanja vya ndege na kuboresha usafiri wa anga na usafirishaji,
- Kukarabati na kupanua bandari, ikiwemo kuboresha mkondo wa Dar es salaam, kuanza ujenzi wa kituo cha shehena ya mizigo Kisarawe, bandari ya Mbegani Bagamoyo, na magati yenye kina kirefu katika bandari ya Tanga na kuipandisha hadhi bandari ya Mtwara,
- Ujenzi wa barabara na madaraja, na
- Kuendelea kutekeleza mpango wa kupunguza msongamano wa magari Dar es Salaam.

D. Kuhakikisha Nishati inakuwepo nchini kwa:

- Kumalizia ujenzi wa mitambo ya Megawati 100 na Megawati 60 Dar es Salaam na Mwanza kwa pamoja, na
- Kuiwezesha TANESCO kununua mitambo ya kufua umeme, serikali ikishirikiana na wawekezeji katika kuendesha mitambo ya Megawati 300 Mtwara, kujenga njia ya umeme yenye msongo wa kilovolti kati ya Morogoro – Tanga – Kilimanjaro na upanuzi wa gridi ya umeme ya kaskazini magharibi kwa mikoa ya Kagera, Kigoma na Rukwa.


E. Kuboresha huduma ya maji kwa:

- Kukarabati mifumo ya maji ili kupunguza uvujaji na upotevu wa maji,
- Kujenga mifumo mipya ya maji na njia za usambazaji, na
- Kujenga Bwawa la Kidunda ili kuboresha huduma ya kusambaza maji katika jiji la Dar es Salaam.

F. Kuimarisha majukumu mengine ya Serikali kama vile:

- Kuimarisha utawala bora na uwajibikaji, na
- Kudumisha amani, utulivu na usalama wa watu na mali zao.

**Mgawanyo wa kisekta kama asilimia ya bajeti nzima**




Kutokana na malengo haya, vipaumbele vya bajeti ya mwaka 2010/2011 ni: upatikanaji wa nishati ya umeme, maji, kuboresha miundombinu ya usafiri na usafirishaji, kuendeleza kilimo na umwagiliaji na kuanzisha ajira katika sekta binafsi na sekta ya umma.

## 3. Vyanzo vya Mapato

Kiasi cha fedha ambacho kimepangwa kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ni shilingi bilioni 13, 526 ambazo ni takribani shilingi trilioni 13.5. Serikali imepanga kupata fedha hizo kupitia; mapato ya ndani (kodi na mapato yasiyo ya kodi), mikopo (fedha kutoka vyanzo vya ndani) pia misaada na mikopo kutoka nje kupitia Washirika wetu wa Mendeleo (vyanzo vya mapato ya nje).

Mchoro uliopo hapa chini unaonyesha michango inayotokana na vyanzo vilivyotajwa hapo juu.

**Chanzo cha Fedha na Kiasi Chake**



## 4. Namna fedha ilivyopangwa kutumika


Matumizi ya bajeti ya Serikali imegawanyika kama ifuatavyo:

a) **Matumizi ya Kawaida**, hii ni jumla ya fedha ambayo Serikali inatumia katika uendeshaji wa shughuli zake. Matumizi haya yanajumuisha gharama za mishahara kwa watumishi wa umma, malipo ya riba ya mikopo ambayo Serikali ilichukua, pango la ofisi na gharama za mafuta n.k.


b) **Matumizi ya Maendeleo,** hizi ni fedha ambazo zitakazotumika kugharamia miradi ya maendeleo kama vile kujenga shule, hospitali na barabara ambapo itasaidia uboreshwaji wa utoaji huduma kwa mwananchi wa kawaida. Matumizi haya yanahusisha kuonekana kwa mabadiliko katika ubora wa maisha.


Mchoro uliopo hapa chini unaonyesha matumizi ya serikali kutokana na vyanzo vilivyobainishwa hapo juu:

**Namna Serikali ilivyopanga kutumia fedha iliyokusanya**



**Matumizi ya Kawaida na Maendeleo katika asilimia ya Bajeti yote.**



## 5. Mabadiliko ya kisera katika kuwezesha bajeti ya 2011/2012

Kwa mtazamo wa kuimarisha ukusanyaji wa mapato, huku tukiboresha hali ya maisha, Serikali inapendekeza mabadiliko yafuatayo:


| Mabadiliko yanayolenga kuendeleza KILIMO kwanza |
|---|

Mabadiliko katika sheria ukusanyaji wa kodi ya mapato:

- Kusamehe kodi kwenye vipuri vya mashine za kukata nyasi na kukaushia mpunga, matrekta, trekta ndogo za kulimia, mashine za kupandia mazao, mashine za kupukuchua nafaka, zana zinazotumika kutengeneza neti za kuvulia samaki, vipuri vya kupulizia madawa, mashine za kupiga haro na mashine za kuchanganyia nafaka.

Mabadiliko katika Sheria ya Kodi ya mapato SURA 332:

- Kusamehe kodi zinazotozwa kwenye kusafirisha samaki nje ya nchi ili kukuza kiwango cha mauzo ya samaki nje ya nchi hivyo kuongeza mapato ya fedha ya kigeni kutokana na sekta hii.



## Mabadiliko yanayolenga kuendeleza Elimu na fursa za ajira

Sheria ya Elimu ya Ufundi Stadi; SURA 82

- Mabadiliko ya mgao wa mapato yanayotokana na tozo kwa ajili ya kuendeleza stadi ya asilimia 6 ili asilimia 4 igawiwe kwenye Bodi ya Mikopo ya Elimu ya juu na asilimia 2 kwa ajili ya Mamlaka ya Mafunzo na Elimu (VETA)ili kuhakikisha kuwa kuna rasilimali fedha ya kutosha katika kutoa mikopo ya Elimu ya juu.

## Mabadiliko mengine yenye kulenga uwezeshaji

Mabadiliko katika Sheria ya Ushuru wa Bidhaa SURA 147,

- Kupunguza ushuru wa bidhaa wa kwenye Mafuta Mazito kutoka shilingi 80 hadi 40 kwa lita ili kupunguza gharama za uzalishaji na kukuza viwanda hivyo kukuza uzalishaji viwandani;
- Kubadili asilimia 120 ya ushuru wa bidhaa uliowekwa kwenye mifuko ya plastiki kwa zaidi ya mikroni 30 ya polymen na kwa asilimia 50.
- Kurekebisha viwango maalumu vya ushuru wa bidhaa zisizo za mafuta ya petroli kwa asilimia 10.

Sheria ya Ushuru wa stempu; SURA 189

- Kusamehe ushuru wa stempu kwenye uhalalishaji wa umiliki wa mali kupitia chombo maalumu cha Uwekezaji kwa lengo la kutoa hati fungani zenye dhamana ya mali.

Sheria ya tozo la Mafuta na Barabara, SURA 220

- Kusamehe tozo la kodi kwenye mafuta yatumikayo katika vyombo, majukwaa na vifaa vingine vinavyotumika katika utafutaji wa mafuta na gesi.
- Kuanzisha akaunti maalumu kupitia TRA ambapo makampuni ya uchimbaji madini yatatakiwa kutoa mpango wa matumizi ya mafuta ya petroli kwa mwaka na kisha kuweka amana ya fedha katika akaunti hiyo kulingana na makadirio ya kodi ya mazao ya petroli itakayotumika katika kila kipindi cha mwezi husika.

Sheria ya Leseni ya Biashara, SURA 208

- Kwa mamlaka za miji (majiji, manispaa na miji) kutoza shilingi 50,000 kwa mwaka kwa biashara yoyote inayofanyika katika eneo husika (isipokuwa vinywaji vikali).
- Halmashauri za wilaya zitatoza na kukusanya ada za leseni za biashara ya shilingi 30,000 kwa mwaka, hii ni kwa biashara ya aina yoyote inayofanyika katika eneo husika.
- Halmashauri za vijiji zitatoza na kukusanya ada ya leseni ya biashara ya shilingi 10,000 kwa mwaka, kwa kila biashara.
- Kurekebisha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ili kujumuisha mabadiliko yaliyopendekezwa hapo juu.

## 6. Mgawo wa Kisekta na Mipango ya Matumizi katika mwaka 2011/2012

Ifuatayo inaonesha bajeti ya kila sekta ikifutiwa na maelezo mafupi ya matumizi ya mipango ya sekta hiyo. JAMBO LA KUZINGATIA, takwimu zinawasilisha tarakimu zinazoonyesha mgao wa kisekta na sio wa kiwizara.

| Sekta ya Elimu |
|---|

Mgao wa Bajeti kwa Sekta .
Bajeti iliyotengwa kwa sekta ya Elimu kwa mwaka 2011/12 ni shilingi bilioni 2,283 ambayo ni ongezeko la asilimia 11.68 kutoka shilingi 2,045.4 bilioni zilizotengwa mwaka 2010/11.


- Shilingi bilioni 954.8 ni kwa ajili maendeleo ya elimu ya msingi,
- Shilingi bilioni 480.7 ni kwa ajili ya maendeleo ya elimu ya sekondari,
- Shilingi bilioni 35.8 ni kwa ajili ya kuwajengea uwezo Waalimu.
- Elimu isiyo rasmi,
- Kuzindua na kutekeleza programu ya “Ndiyo Naweza” ili kupunguza ujinga, wa kusoma na kuandika,
- Kufanya tathmini ya kiwango cha ujinga wa kusoma na kuandika.

Elimu ya Juu

- Kulipia wanafunzi 1,900 wanaochukua shahada ya kwanza ya Udaktari
- Kulipia wakufunzi 120 katika masomo ya shahada za uzamili
- Kuwadhamini wanafunzi 126 wa vyuo vikuu wanaosoma Uganda na Msumbiji kupitia programu ya kubadilishana wanafunzi.
- Kuwalipia walemavu 112 katika elimu ya juu
- Kukiwezesha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuanzisha Kituo cha Taaluma kama sehemu ya kuazimisha miaka 50 ya Taasisi hiyo.
- Chuo cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere kuanzisha programu za stashahada na shahada katika ugharimiaji elimu kwenye kampasi ya Bububu- Zanzibar

Elimu ya Ufundi Stadi

Ili kutatua tatizo la uwezo na masuala ya ustawi, Serikali imetenga kiasi cha shilingi 278 bilioni kiasi ambacho ni sawa na asilimia 2 ya tozo la maendeleo ya ufundi stadi kwa ajili ya kuendeleza mafunzo ya ufundi stadi.



## Sekta ya Afya


Sekta ya Afya kwa mwaka 2011/12 imetengewa kiasi cha shilingi 1,209.1 bilioni ambacho ni ongezeko la asilimia 0.3 ikilinganishwa na shilingi 1,205.9 bilioni zilizotengwa mwaka 2010/11

a. Mipango ya matumizi katika sekta

- Shilingi bilioni 20 zimetengwa kupitia programu ya Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) kwa ajili ya kujenga zahanati vijijini kwa nchi nzima ili kuboresha na kuimarisha huduma ya afya ya msingi.
- Shilingi bilioni 189.6 zimetengwa kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma ya afya ya msingi katika ngazi ya wilaya katika kununua na kugawa madawa na vifaa vya tiba. Fedha hizo pia zitatumika kuwajengea uwezo watumishi wa afya (Wauguzi, Madaktari, Wakunga) katika ngazi hiyo ya Wilaya.
- Shilingi bilioni 6.6 zimetengwa kwa ajili ya kukarabati na kuzifanyia matengenezo hospitali za wilaya kwa nchi nzima. Nyongeza ya shilingi bilioni 4.5 zimeelekezwa kwenye miradi inayoendelea ya ujenzi wa hospitali za Singida, Shinyanga, Mbeya na Manyara wakati shilingi bilioni 5.6 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo na maboresho ya hospitali zilizopo nchi nzima.
- Shilingi bilioni 22.6 zimetengwa kutekeleza mipango ya kupunguza vifo vya watoto chini ya miaka mitano na akina mama. Fedha hizi pia zitatumika katika kusambaza vitamini A na D, na vifaa 100,000 vya kuwasaidia akina mama wakati wa uzazi.
- Shilingi bilioni 87 zimetengwa katika programu za kudhibiti Kifua Kikuu (TB) na Ukoma, na magonjwa mengine ya kuambukiza kwa nchi nzima. Fedha hizi zitalenga zaidi katika kuimarisha huduma za kinga.
- Shilingi bilioni 76.1 zimetengwa katika huduma za tiba ambapo shilingi bilioni 2.5 zitaelekezwa kwenye matibabu ya Kansa.
- Shilingi bilioni 1.4 zimetengwa ili kusaidia watu wenye Ulemavu, Wazee na Yatima.

- Katika kupambana na kuzuia VVU na UKIMWI, serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 127.1 kusambaza dawa za ARVs, kununua mashine 150 za kupima CD4 ili kutoa huduma kwa watu wanaoishi na VVU na UKIMWI. Fedha hizi pia zitatumika katika kuongeza vituo 400 vya kutolea huduma kwa watu wenye VVU.

- Shilingi bilioni 85.5 zimetengwa kwa ajili ya kutoa huduma ya Bima ya Afya.




## Sekta ya Maji

a. Bajeti iliyotengwa kwa Sekta

Sekta ya maji kwa mwaka wa 2011/2012 imetengewa shilingi bilioni 621.6 ambazo ni ongezeko la asilimia 56 ikilinganishwa na shilingi bilioni 397.6 zilizotengwa mwaka 2010/11.

b. Mipango ya matumizi katika sekta

- Shilingi bilioni 86.7 zimetengwa kwenye Halmashauri na Sekretariati za Mikoa kwa ajili ya kujenga miundombinu ya maji katika Vijiji 10 vya kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa,

- Shilingi bilioni 7.033 zimetengwa kwenye ujenzi wa mabwawa na uchimbaji wa visima katika wilaya za Chamwino, Nkasi, Chunya, Bunda, Rorya, Musoma, Kishapu, Bariadi, Iringa na Meatu,
- Shilingi bilioni 106.7 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maji katika manispaa za Musoma na Bukoba,
- Shilingi bilioni 6 zimetengwa katika utekelezaji wa mradi wa maji katika jiji la Dodoma,
- Shilingi bilioni 8.6 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maji Manispaa ya Morogoro,
- Shilingi bilioni 6 zimetengwa kwa ajili ya kuboresha mfumo wa huduma za maji safi na taka Dar es Salaam na ujenzi wa bwawa la Kidunda, na
- Shilingi bilioni 24.6 zimetengwa kwa ajili ya chujio la maji huko Ruvu Chini.

## Sekta ya Kilimo

a. Mgawo wa bajeti kwa Sekta

Bajeti ya sekta ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ni shilingi bilioni 926.2 ambayo ni ongezeko la asilimia 2.5 kutoka shilingi bilioni 903.8 iliyotengwa mwaka wa fedha 2010/2011.

b. Mipango ya matumizi katika sekta

Sekta inapanga kushughulikia changamoto kubwa zinazoathiri maendeleo ya Kilimo nchini ikiwemo kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji, utoaji wa huduma ya mikopo kwa wakulima, kuongeza tija, kuboresha miundo mbinu ya masoko na kuchukua hatua za kupunguza athari ya mabadiliko ya tabia nchi.

Hatua zinazochukuliwa ni pamoja na;

- Kutenga shilingi bilioni 7.1 kuwezesha upatikanaji wa pembejeo ikiwemo ununuzi wa matrekta makubwa na matrekta madogo,
- Kutenga shilingi bilioni 136.7 kwa ajili ya kuendeleza utoaji wa ruzuku ya mbolea na madawa kwa mazao mbalimbali,

- Shilingi bilioni 7.3 zimetengwa kwa ajili ya ruzuku za mbegu na miche bora,
- Shilingi bilioni 18.2 zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa chakula na pia kufanya utafiti kwa lengo la kukusanya taarifa ili kubaini hali ya chakula nchini,
- Shilingi bilioni 1.4 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya umwagiliaji. Serikali imedhamiria kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji ambayo inajumuisha miradi 95 ya umwagiliaji kufikia hekta 70,500,
- Shilingi bilioni 6.5 zitaelekezwa kwenye utoaji wa elimu na huduma za ugani, utawanyaji wa teknolojia ikiwemo ya ugani wa kati ya mkulima na mkulima. Fedha hizi pia zitatumika katika miundombinu ya vyuo vya kilimo,
- Shilingi bilioni 4.5 zimetengwa kwa ajili ya kuimarisha utafiti wa mbegu bora ambazo zinahimili vidudu viatilifu na magonjwa, ukame na pia kutoa mazao mengi. Fedha hizi pia zitatumika katika kufanya tafiti juu ya kutafuta njia mbalimbali za kuhifadhi rutuba ya udongo,
- Shilingi bilioni 10.9 zimetengwa kuboresha tija katika uzalishaji wa zao la mpunga ikiwemo kulifanya zao hilo kuwa la kibiashara zaidi, kwa kutoa zana za kulimia, kuvunia na mfumo wa masoko,
- Shilingi bilioni 1.9 zimeelekezwa katika kutekeleza maboresho na kuimarisha vyama vya ushirika vikiwemo vyama vya msingi vya kuweka na kukopa (SACCOS),
- Shilingi bilioni 2.1 zimetengwa kwa ajili ya kuboresha machinjio, kuwajengea uwezo, kusindika ngozi za wanyama wakubwa na wadogo, na
- Shilingi bilioni 13.2 ni kwa ajili ya kuboresha hifadhi ya mazingira ikiwa ni pamoja na usimamizi wa sheria, elimu kwa umma, na usimamizi endelevu.



**Ufugaji bora mbuzi wa asili katika Wilaya ya Kondoa**

## Sekta ya Nishati

a. Mgawo wa bajeti katika sekta

Sekta ya Nishati katika mwaka 2011/2012 imetegewa bajeti ya shilingi bilioni 539.3 ambayo ni ongezeko la asilimia 65 ikilinganishwa na shilingi 327.2 bilioni zilizotengwa mwaka wa fedha wa 2010/2011.

b. Mipango ya matumizi katika sekta

- Shilingi bilioni 124.9 zimetengwa kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa mitambo ya dharura ya umeme ambayo itafua Megawati 100 jijini Dar es Salaam na Megawati 60 jijini Mwanza,
- Shilingi bilioni 136.9 zimetengwa ili kutekeleza programu nyingine maalumu za kuboresha miundombinu na usafirishaji wa umeme,
- Shilingi bilioni 54.2 zimetengwa kwa ajili ya Wakala wa Umeme Vijijini (REA) na Mfuko wa Umeme Vijijini ambao utaongeza uwekezaji katika umeme vijijini ambao utawezesha wananchi kuanzisha shughuli zaidi za kiuchumi Vijijini na hivyo kuongeza fursa za ajira,

- Shilingi bilioni 6.6 zimetengwa ili kuwekeza na uendelezaji wa gesi asilia ya Songo Songo na Ghuba ya Mnazi (Mnazi Bay) ili kuongeza uzalishaji wa gesi kwa ajili ya matumizi viwandani na majumbani, na
- Shilingi bilioni 6.5 zimetengwa kwa ajili ya kukuza maendeleo ya sekta ndogo ya petroli nchini.



**Mtambo wa Megawati 100 za umeme kutokana na gesi asilia Ubungo, Dar Es Salaam.**

## Sekta ya Miundombinu

a. Bajeti iliyotengwa katika sekta

Jumla ya shilingi 2.78 trilioni zimetengwa kwa ajili ya miundombinu ya barabara na usafirishaji, TEHAMA, Utafiti na Maendeleo mahsusi ajili ya miundo mbinu ya barabara, reli, bandari na viwanja vya ndege. Bajeti ya mwaka 2011/12 imeongezeka kwa asilimia 85 ikilinganishwa na shilingi bilioni 1,505.1 zilizotengwa mwaka wa fedha wa 2010/11.

b. Mipango ya matumizi katika sekta

- Shilingi bilioni 112 zimetengwa kwa ajili ya kujenga miundombinu ya viwanja vya ndege,
- Shilingi bilioni 123 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati

wa miundombinu ya reli, ikijumuisha ununuzi na ukarabati wa mabehewa,

- Shilingi trilioni 1.7 zimetengwa ili kugharamia ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya barabara ikiwa pamoja na ununuzi na ukarabati wa vivuko, na
- Shilingi bilioni 5 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Serikali.

Kuhusiana na kuimarisha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Utafiti na Maendeleo (R&D), Serikali katika mwaka wa fedha wa 2011/12 imetenga;

- Shilingi bilioni 2 kwa ajili ya Mkongo wa Taifa wa TEHAMA
- Shilingi bilioni 25.9 kwa ajili ya kugharamia Utafiti na Maendeleo

## Kuongeza fursa za Ajira

Serikali imepanga kutumia shilingi milioni 140 kwa programu za kuongeza fursa za ajira kwa nchi nzima.

- Shilingi milioni 700 zimetengwa kwa ajili ya Mradi wa Mfuko wa Uwezeshaji wa Mwananchi ili kugharamia miradi ya kuwawezesha vijana kujiajiri wenyewe,
- Shilingi milioni 2 zimetengwa ili kuwezesha utekelezaji wa Mradi wa Kumwezesha Mwanamke Kiuchumi ambao unanuia kuwawezesha wanawake Tanzania,
- Shilingi milioni 925 zitatolewa kama mkopo kwa wajasiriamali wadogo nchini kupitia vyama vya msingi vya kuweka na kukopa(SACCOS), na
- Shilingi milioni 500 zimetengwa kwa ajili ya Mfuko Dhamana wa Rais (PTF) ili kusaidia wajasiriamali wadogowadogo nchini.

## Sekta ya Uzalishaji na Viwanda

- Shilingi bilioni 4.5 zimetengwa kwa ajili ya Mpango wa Maeneo Maalum ya Kiuchumi (SEZ) ikiwa pamoja na kulipa fidia kwa ardhi iliyotengwa kwa ajili ya maeneo hayo,
- Shilingi bilioni 4.8 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanda cha Dawa za Kuua Viluwiluiwi vya Mbu. Hatua hii itasaidia kupunguza mbu wanaoneza malaria,
- Shilingi bilioni 4.5 imetengwa ili kusaidia Programu ya Wajasiriamali Wadogo wadogo, Wadogo na wa Kati Vijijini (MUVI) ambao umelenga kuboresha fursa za ajira katika mikoa sita ya Tanga, Pwani, Manyara, Ruvuma, na Mwanza, na
- Shilingi bilioni 1.8 zimetengwa kwa ajili kuongeza shughuli za ujasiriamali. Kati ya kiasi shilingi bilioni 1 zimepangwa kutumika katika Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Ujasiriamali (NEDF) ambao unatafuta namna ya kuzidisha uwezo wajasirimali wadogo wadogo kupata mikopo.

## Nyaraka Rejea za Bajeti

Ifuatayo ni orodha ya nyaraka za serikali zinazotumika kama chanzo cha taarifa kwa ajili kuandaa bajeti:

- Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025;
- Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16)
- Mfumo wa Sera za Uchumi Jumla; unatoa taarifu juu ya sera za kodi na maboresho
- Malengo ya Taifa ya MKUKUTA Awamu ya Pili (2010 hadi 2015); ambao umelenga kutumia ukuaji wa uchumi kama njia ya kukabiliana na umaskini na unatilia mkazo juu ya jukumu la sekta ya kilimo.
- Malengo ya Mendeleo ya Milenia , 2015: yanalenga kukabiliana na njaa, elimu, usawa wa jinsia, afya ya mama na mtoto, kupambana na Virusi Vya Ukimwi na Ukosefu wa Kinga Mwilini, mazingira endelevu na kukuza ushirikiano wa kimataifa.
- Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ( 2010-2015);
- Mfumo wa Sera za Uchumi Mkuu; unatoa taarifa juu ya sera za kodi na maboresho.
- Mkakati wa Pamoja wa Misaada Tanzania;
- Sera na Mikakati ya Kisekta;
- Mkakati wa Deni la Taifa;
- Hotuba za Bajeti za Wizara;
- Hotuba ya Hali ya Uchumi wa Nchi;
- Mchakato wa Mapitio ya Matumizi ya Serikali;
- Muswada wa Sheria ya Fedha 2011;
- Muswada wa Sheria ya Matumizi 2011;
- Mchakato wa Mapitio ya Matumizi ya Serikali;

- Mfumo wa Tathmini ya Utendaji (PAF) wa Serikali na Washirika wa Maendeleo chini ya GBS;
- Mfumo wa Muda wa Kati wa Matumizi ya Serikali;
- Vitabu vya Makisio ya Mapato na Matumizi ya Serikali (Juzuu Na. 1 – IV)

Utaweza kufanyia nini taarifa hii?
Bajeti ya Serikali ni kielelezo muhimu kinachoonesha mipango thabiti ambayo Serikali imepanga kufanya katika mwaka huo. Kama unataka kujua kodi yako inakwenda wapi, na kama kuna mipango ya kuboresha elimu au afya katika eneo lako, na unaweza ukaangalia kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa ajili ya maendeleo. Kijitabu hiki kinajaribu kutoa taarifa kwa muhtasari katika lugha nyepesi iwezekanavyo. Hata hivyo, unaweza kupata taarifa zaidi juu ya mchakato wa bajeti kutoka katika vyanzo vifuatavyo:

- Nyaraka za bajeti ya Serikali (angalia Nyaraka za Rejea za Taarifa hii) na husasan Juzuu Nne za Makisio ya Bajeti ya Serikali ambazo zinapatikana katika Wizara ya Fedha:
- Wizara ya fedha, S.L.P 9111, Dar es Salaam (Tovuti: http://www.mof.go.tz)
- Ofisi za Serikali za Mitaa na/au Viongozi katika eneo lako kama vile Mwenyekiti au Mtendaji wako,
- Policy Forum, S.L.P 38486, Dar es Salaam.

Kumbuka kuwa ni haki yako kujua taarifa hii na nyingine zaidi kuhusiana na bajeti ya Serikali Zungumzeni na viongozi wenu kuhusu taarifa hii na pia wajulishe watu wengine katika jamii yenu!

(unaweza kuchana ukurasa huu)

Je, una mawazo, maswali au maoni gani kuhusiana na bajeti hii?

- Je ungetaka kupata taarifa zaidi ya hii iliyotolewa katika kijitabu hiki? Ni taarifa ya aina gani ungehitaji?

- Je kuna kitu kingine zaidi ambacho ungetaka sisi tujue?

1. Je, kijitabu hiki kimekuwa na manufaa
   ☐ Ndiyo ☐ Hapana ☐ Kwa kiasi

2. Je kijarida hiki kimesomeka kwa urahisi na kueleweka
   ☐ Ndiyo ☐ Hapana ☐ Kwa kiasi

Tuma au fikisha kikatarasi hiki kwa, Kamishna, Idara ya Bajeti ya Serikali, Wizara ya Fedha S.L.P. 9111, Dar es Salaam

**Wasiliana nasi:**

## Wizara ya Fedha

S.L.P 9111,
Dar es Salaam
Tanzania
Simu: +255 22 211 1174-6
Nukushi: +255 22 211 0326
Tovuti: www.mof.go.tz